

Mambo yahusianayo na afya



Cytomegalovirus (CMV) Retinitis

CMV Retinitis Ni Nini?

- CMV retinitis ni mambukizo ugonjwa mbaya unaoshambulia jicho na unaweza sababisha upofu. Mashambulizi haya husababishwa na kijidudu kinachoitwa CMV (cytomegalovirus).
- Watu wenye maambukizi ya vijidudu vya ukimwi na kipimo cha CD4 chao kilicho chini ya 50 huwa hatarini zaidi katika kupatwa na hali hii.

Jinsi Gghani Mtu Hupatwa Na CMV?

- CMV ni kijidudu kilicho cha kawaida sana. Watu wengi huweza kuwa wamekumbana nacho mara kadhaa maishani mwao. Kwa kawaida hakileti madhara yeyote kwa mtu mwenye mfumo wa kupigana na magonjwa ulio imara.
- Kwa watu wenye mfumo wa kupigana na magonjwa ulio dhaifu, (kama vile watu wenye vipandikizo kadhaa vya sehemu za mwili (organ transplants), watu walio kwenye matibabu ya kansa kwa kutumia madawa makali, au watu wenye ukimwi), CMV huweza sababisha magonjwa kadhaa mabaya.

Ni Zipi Dalili Za CMV?

- CMV huweza shambulia sehemu tofauti za mwili, kama vile macho, mapafu, tumbo, utumbo na ubongo. Dalili zake hutofautiana, ila sehemu kuu maarufu ambayo CMV hushambulia mwilini ni kwenye macho.



Canadian AIDS Treatment
Information Exchange
Réseau canadien
d'info-traitements sida

www.catie.ca



www.apaa.ca

Maamuzi juu ya matibabu ya aina mbalimbali yanahitajika kufanywa kwa kushauriana na mtaalamu aliyehitimu kwenye mambo ya afya na mwenye ujuzi juu ya magonjwa yanayoendana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi na matibabu atakayoamuliwa kutumiwa.

CMV Retinitis

- CMV retinitis inapotokea, retina (mboni ya jicho?) hushambuliwa na CMV. Dalili zake huweza kuwa pamoja na kutoana vitu sawasawa, kuona vitu nusununu (alama nyeusi huonekana kutembea machoni mwako). Kwa kawaida hutasikia maumivu yeyote, ila hali huweza badilika kwa haraka na kusababisha upofu. Ni muhimu kumweleza daktari wako mabadiliko yeyote ya ufanisi wa macho yako ili aweze kukuanzia matibabu mapema.

Nawezaje Kuinga CMV Retinitis?

- Kwa kuwa CMV hushambulia watu wenye mfumo wa kupigana na magonjwa ulio dhaifu (wenye kipimo cha CD4 chini ya 50), njia kuu ya kuzuia CMV ni kuwa na afya bora na kuhakikisha chembecheme zako za CD4 zipo kwenye kiwango cha juu.
- Dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi huweza saidia kuhimarisha afya yako na kufanya mfumo wako wa kupigana na magonjwa kuwa mzuri na hivyo kuwezesha kipimo chako cha CD4 kuwa juu.
- Mazoea ya kutazama na kujuwa juu ya afya yako kutoka kwa daktari wako au mtaalamu wa macho pia huweza saidia kugundua CMV retinitis mapema.

Jinsi Ghani CMV Retinitis Inaweza Kutibiwa?

- Matibabu ya CMV retinitis kwa kawaida hutolewa kwa kutumia sindano yenye dawa husika kupitia kwenye mshipa (IV) au moja kwa moja kwenye jicho/macho yaliyoshambuliwa na CMV.
- Dawa zinazotumika kutibia CMV ni kama:
 - ganciclovir (Cytovene) na valganciclovir (Valcyte)
 - foscarnet (Foscavir)
 - cidofovir
- Dawa hizi huziui kijidudu cha CMV, bali hucheleweshwa usambaaji wa CMV mwilini mwako. Matibabu haya hufanyika kwa kipindi chote cha maisha yako. Kwa dawa zinazohitajika kutumika kwa kutumia vishipa vya mwili, mara nyingi watu huwekewa njia ya kudumu ya kuingizia dawa kwenye kijishipa cha mwili ili



CMV Retinitis

waweze pokea dawa zao kila siku. Wakati mwingine watu huweza tumia dawa zilizo kwenye mfumo wa vidongo za ganciclovir au valganciclovir kuendelea kujiimarisha baada ya kuhakikisha kuwa maambukizi yamesitishwa.

- Kutokana na maendeleo katika ugunduzi wa matibabu ya maambukizi ya vijidudu vya ukimwi, watu wengine hupata nafuu na kuongeza viwango vyao vya CD4 na afya zao kwa ujumla hata kuweza acha kutumia dawa za CMV kwa kipindi fulani. Ongea na daktari wako juu wa uwezekano huu.

Shirika la kubadilishana maelezo juu matibabu ya ukimwi Kanada (The Canadian AIDS Treatment Information Exchange – CATIE) na Shirikisho la waafrika katika kupigana na ukimwi (Africans in Partnership Against AIDS - APAA) kwa nia nzuri kabisa wanatoa maelezo kwa watu wanaoishi na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi/Ukimwi ambao wangependa kutawala afya zao wenyewe kwa kushirikiana na wataalamu wa afya wanaowapatia matibabu. Hata hivyo, maelezo haya yanayochapishwa au kutolewa na CATIE au APAA hayawezi kuchukuliwa kama ushauri wa kiafya. Hatushauri au kusisitiza juu ya tiba moja juu ya nyingine. Hivyo tunawashauri watumiaji ya maelezo yetu kupitia maelezo ya matibabu mengine yanayotolewa na vyanzo mbalimbali kwa upeo mkubwa iwezekanavyo. Tunawashauri watumiaji wa maelezo haya na kusisitiza kuwa ni muhimu kushauriana na wataalamu wa afya na tiba waliohitimu mafunzo yao kabla ya kuamua, kutumia au kuanza jambo lolote juu ya matibabu.

Vile vile, hatuthibitishi au kudhamini ukweli au ufarisi na ujuzi wa maelezo yanayochapishwa au kupatikana kutoka CATIE au APAA. Watumiaji wanaotumia au kutegemea maelezo haya wanafanya hivyo kwa kuthubutu wenyewe na matokeo yake yakiwa mabaya yatakuwa juu yao. Si CATIE wala APAA, au Wizara ya Afya Kanada, au wafanyakazi wao, wakurugenzi, maafisa au watu wanaojitolea wataweza kuhusishwa na uharibifu wa aina yeyote unaoweza kutokea kwa kutumia vizuri au vibaya maelezo haya. Mawazo na maelezo yaliyotolewa hapa au kwenye nakala yeyote au ilani/tangazo lolote.

Copyright: This Fact Sheet is made available through a collaboration between Africans in Partnership Against AIDS (APAA), Asian Community AIDS Services (ACAS) and the Canadian AIDS Treatment Information Exchange (CATIE). Original content developed by ACAS, 2001. Translation into Swahili and Hausa by APAA, 2004.

This information is also available in Chinese, Tagalog and Vietnamese

Funding has been provided by Health Canada, under the Canadian Strategy on HIV/AIDS

Supported by an unrestricted educational grant from GlaxoSmithKline in partnership with Shire BioChem



partnership
in partnership with

